MINISTÈRE
DE L'EUROPE
ET DES AFFAIRES
ÉTRANGÈRES
*Liberté*
*Égalité*
*Fraternité*

DIRECTION GENERALE DE L'ADMINISTRATION
ET DE LA MODERNISATION

DIRECTION DES RESSOURCES HUMAINES

Sous-direction de la politique des ressources humaines

Bureau des concours et examens professionnels

# CONCOURS EXTERNE ET INTERNE POUR L'ACCÈS AU CORPS DES ADMINISTRATEURS DE L'ÉTAT DÉNOMMÉS « CONCOURS D'ORIENT » AU TITRE DE L'ANNÉE 2024

---

**ÉPREUVES ÉCRITES D'ADMISSIBILITÉ**

**Mercredi 6 septembre 2023**

## SWAHILI

Durée totale de l'épreuve : 3 heures
Coefficient : 2
Toute note inférieure à 10 sur 20 est éliminatoire
Barème de notation : composition en swahili 12 points ; traduction en français 8 points

**TRADUCTION EN FRANÇAIS**

*Traduction en français d'un texte rédigé en swahili*

TEXTE AU VERSO

**Consigne : traduire uniquement les parties grisées (372 mots en tout)**

BBC 8 Juni 2023

## Upi umuhimu wa bandari ya Dar es Salaam?

Na Rashid Abdallah, mchambuzi Tanzania

Mjadala juu ya bandari ya Dar es Salaam, Tanzania umekuwa mkubwa katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, baada ya serikali ya Tanzania, kuonesha azma ya kutaka kuingia makubaliano ya kuipa kandarasi kampuni ya DP World kutoka Umoja wa Falme za Kiarabu kusimamia bandari hiyo.

Kwa mujibu wa msemaji mkuu wa serikali ya Tanzania, Gerson Msingwa akizungumza na BBC, makubaliano ya awali ya kushirikisha kati ya pande hizo mbili ndio yamesainiwa. Lakini bado hayajatiwa saini ya mwisho kuhusu vipengele vya namna gani makubaliano hayo yatafanyika.

Kwa kuzingatia ukubwa wa jambo lenyewe, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania litatakiwa kujadili jambo hilo, baada ya wananchi kutoa maoni yao (...).

### Umuhimu wa bandari ya Dar

Bandari ya Dar es Salaam ndio kuu nchini Tanzania, haitoi huduma kwa Tanzania pekee. Nchi jirani zisizo na bahari zinatumia bandari hiyo vilevile; Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Burundi, Rwanda, Malawi, Uganda na Zimbabwe.

Kwa mujibu wa tovuti ya bandari hiyo, asilimia 95 ya biashara za kimataifa za Tanzania, zinahudumiwa na bandari Dar es Salaam. Bandari hiyo inaunganisha Mashariki ya Kati, Mashariki ya Kati, Ulaya na Marekani.

Mwaka 2019/2020 makusanyo ya bandari ya Dar es Salaam, yalikuwa shilingi bilioni 901, mwaka 2020/2021 ilikusanya shilingi bilioni 896, na mwaka 2021/2022 katika robo ya kwanza ilikusanya shilingi bilioni 980 hadi mwisho wa mwaka.

Hadi hapo mambo yanaonekana kwenda vizuri. Ila upande mwingine, bandari hii ina changamoto zake vilevile - nyingine ni za muda mrefu. Bandari ya Dar es Salaam ni moja ya eneo ambalo hayati Rais John Pombe Magufuli alifanya ziara ya kushtukiza baada tu ya kuingia Ikulu, katika kipindi chake cha kwanza cha miaka mitano - ziara za kushutukiza bandarini ziliendelea na kila wakati alikutana na matatizo (...)

Katika kipindi cha mwongo mmoja uliopita takribani wakurugenzi sita wa bandari ya Dar es Salaam wameteuliwa na kutumbuliwa, kwa sababu mbali mbali - ukiwemo utendaji mbovu na ubadhirifu wa fedha (...)

### Bandari ya Dar Inaweza kubinafsishwa?

Lengo la serikali kuipa mwekezaji bandari ni ili kuongeza ufanisi na mapato, kwa mujibu wa Msigwa, ufanisi wa bandari hiyo kwa sasa ni mdogo. Ukiachilia maelezo ya serikali, kuna maswali mengi yanayoulizwa, moja wapo ni ikiwa kuna faida kwa Tanzania kuibinafsisha bandari yake kuu.

Ubinafishaji ni hatua ya mali kutoka kwenye mikono ya serikali na kwenda kwa mtu au kampuni binafsi inaweza kuwa ya ndani ama ya nje. Na mantiki yake ni kuisaidia serikali kukusanya pesa, kuongeza ufanisi wa shughuli zitokanazo na ubinafsishaji huo na hatimaye kukuza uchumi wa nchi kutokana na ongezeko la mapato.

Nimemwuliza Mhadhiri na Mchumi kutoka Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Tanzania, Beatrice Kimaro, ni mambo gani muhimu ya kuzingatia ikiwa serikali inataka kubinafsisha mali?

“Serikali inapotaka kubinafsisha chochote, kwa mfano mjadala wa bandari Tanzania, ni lazima izingatie maswala haya: Je, itasaidia kuongeza ufanisi? Itasaidia kuongeza mapato na kuchochea uchumi wa nchi? Ikiwa maslahi ya nchi husika na watu wake hayaonekani, hakuna mantiki ya kubinafsisha.”

“Mwaka 2016, Serikali ya Australia ilibinafsisha bandari ya Melbourne kwa mwekezaji kwa miaka 50 kwa thamani ya dola bilioni 9.7, leo ni moja ya bandari kubwa nchini humo kwa uingizaji na usafirishaji wa shehena za mizigo,” amefafanua Beatrice na kuongeza:

“La muhimu zaidi ni lazima kuwe na ushirikishwaji wa wazi kwa mchakato wa aina hii kwa sababu jambo kama bandari ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi. Kukishakuwa na muafaka wa pamoja, lazima hatua zote za kisera na kisheria ziongoze mchakato ili kuondoa manung’uniko mbeleni. Na hakuna haja ya kuharakisha zoezi la aina hii kwa sababu ya unyeti wake.”